**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# TAMKO LA SIKU YA MAADHIMISHO YA SIKU YA HEDHI SALAMA DUNIANI LILILOTOLEWA NA MHE. DKT. DOROTHY O. GWAJIMA (MB), WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, ITAKAYOFANYIKA DODOMA, TAREHE 24 MEI, 2021.

**Ndugu Wanahabari,**

Namshukuru mwenyezi Mungu kutukutanisha hapa kuzungumzia suala muhimu la Hedhi Salama. Napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Wanahabari wote kwa ushirikiano wenu kwenye kutekeleza Ilani ya Chama Mapinduzi chini ya **Uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Pia, ninawashukuru kwa kuendelea kushirikiana na jamii nyingine duniani kueneza ujumbe wa Maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama.

**Ndugu Wanahabari,**

Maadhimisho haya yalianza kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka 2013 ambapo yaliasisiwa na Asasi isiyo ya Kiserikali ya Kijerumani iitwayo **WASH United Organization**. Baada ya hapo kumekuwa na mwamko mkubwa kwenye Mataifa mengi Duniani wa kuyatambua maadhimisho haya ambayo kilele chake ni tarehe 28 Mei ya kila mwaka. Aidha, katika kuadhimisha siku hii, kwa ujumla Duniani kunakuwa na jukwaa linalojumuisha wadau mbalimbali pamoja na vyombo vya habari ili kutoa sauti za pamoja juu ya hedhi salama kwa wasichana pamoja na wanawake wote.

**Ndugu Wanahabari,**

Mwaka jana (2020) kutokana na kuibuka kwa janga la COVID-19, maadhimisho haya hayakuweza kufanyika kwa kukutana. Hata hivyo, jumuia ya Kimataifa iliendelea kufahamishana, kuelimishana na kukumbushana juu ya jambo hili muhimu kwa njia ya mtandao. Lengo kuu ni kueleza Dunia na Umma wa Tanzania kuwa hedhi **sio** ugonjwa wala laana bali ni hali ya kawaida na Baraka ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu inayomtokea msichana mara baada ya kuvunja ungo kama ishara ya mabadiliko kwenye mfumo wa maumbile yake ya uzazi. Tafiti zinaonesha kuwa, kila siku wanawake zaidi ya milioni 12 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 wanakuwa kwenye Hedhi duniani.

**Ndugu Wanahabari,**

Napenda kuchukua fursa hii kuelimisha jamii kwa ufupi kuhusu dhana ya hedhi salama. Maana ya Hedhi Salama ni kwamba msichana/mwanamke anapokuwa katika siku zake anatakiwa kuwa katika mazingira salama na kwamba anapata huduma zote muhimu ikiwemo miundombinu ya vyoo vyenye usiri, maji safi, taulo za kike au vifaa salama vya kujisitiri na utupaji salama wa vifaa/taulo za kike zilizotumika. Hivyo, hedhi isiyo salama inaweza kuchangiwa na miundombinu duni ya vyoo, kukosekana kwa maji safi na salama, matumizi ya vifaa vya hedhi visivyo salama na utupaji ovyo wa vifaa vilivyotumika. Vilevile, Hedhi isiyo salama inachangiwa na mambo mbalimbali yakiwemo mitazamo ya imani pamoja na uelewa mdogo wa jamii kwenye suala zima la Afya ya hedhi.

**Ndugu Wanahabari,**

Kwa muktadha huu, Hedhi isiyo salama ina athari mbalimbali za kiafya ambazo ni pamoja na kupata magonjwa kama maambukizi katika mfumo wa mkojo yanayoweza kusambaa zaidi na kupelekea maambukizi kwenye mji wa uzazi na hadi kufikia ugumba. Vilevile, ukiacha athari za kiafya, hedhi isiyo salama inaweza kuathiri maendeleo ya mwanamke katika nyanja zote ikiwemo elimu, uchumi, n.k. **Hivyo, kutokana na ukweli huu, ni matumaini**

**yangu kuwa siku ya leo itatumika vyema kufikisha ujumbe kuhusu hedhi kwa ujumla, hedhi salama na wajibu wa kila mmoja na kila Sekta katika kuhakikisha tunaungana kwa pamoja kuimarisha afya ya hedhi kwa mabinti zetu na wanawake kwa ujumla ili wasikwame katika kushiriki kwenye maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla.**

**Ndugu Wanahabari,**

Matokeo ya utafiti uliofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) pamoja na OR -TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau wa Hedhi Salama mwaka 2019, yanaonesha Nchi yetu imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya ajenda ya afya ya hedhi. Hata hivyo, changamoto ni nyingi katika ngazi ya jamii hususan kuwa na uelewa mdogo wa jamii juu ya hedhi salama. Kwa mfano ni asilimia 28 tu ya wasichana ndiyo wenye uelewa thabiti juu ya hedhi salama. Aidha, ilionekana kuwa wasichana wengi huwa wanapata changamoto ya kumudu gharama za taulo za kike, kupata maji salama na vyoo bora. **Hivyo, jamii bado inatakiwa kupiga hatua kubwa ya kuendelea kutoa elimu shuleni, katika jamii na pia nyumbani ikiwemo kuwashirikisha akina Baba kutambua umuhimu wa hedhi salama kwa ujumla wake.**

**Ndugu Wanahabari,**

Takwimu pia zinaonesha kuwa maeneo mengi hapa Nchini jamii inakosa uelewa wa umuhimu wa hedhi salama. Maeneo yaliyofanyiwa utafiti na kuonesha ukosefu wa uelewa wa hedhi salama ni pamoja na Halmashauri za Namtumbo, Muleba, Mbeya, Igunga, Temeke, Karatu, Tandahimba, Rorya, Kusini Unguja na Kaskazini Pemba ambayo jamii yake ilionekana inauwelewa mdogo juu ya suala la hedhi salama. Hii ina maana kuwa katika mipango yetu, Serikali na Wadau tunatakiwa kuangalia maeneo haya ambayo bado yako nyuma katika kuzingatia suala hili. Vinginevyo, mabinti zetu na wanawake walioko maeneo haya watakuwa nyuma kwa maendeleo kutokana na kukabiliwa na changamoto ya hedhi isiyo salama.

**Ndugu Wanahabari,**

Vile vile, napenda kuzungumzia kikwazo cha imani katika kufikia malengo ya hedhi salama. Baadhi ya jamii wana imani potofu kiasi cha kuwa na unyanyapaa na hivyo kuwa ni ngumu kuweka mipango ya maendeleo ya kuboresha usafi na hedhi salama hapa Nchini. Jamii nyingi zinahusisha hedhi na uchafu au najisi katika masuala ya dini. Aidha, imeripotiwa kuwa, katika baadhi ya maeneo, wasichana au wanawake wanapokuwa kwenye hedhi hawaruhusiwi kugusa vyanzo vya maji, kupika au kuingia jikoni, kuosha vyombo, kugusa mimea au kupita katika mashamba na hawatakiwi kushiriki shughuli za Dini. Hali kadhalika, maumivu ya tumbo wakati wa hedhi huhisiwa kuwa msichana au mwanamke ametoa mimba au amejamiana na mume wa mtu mwingine au anadanganya/anajisingizia.

**Ndugu Wanahabari,**

Kutokana na hali na mila potofu nilizoongelea hapo juu ni wakati muafaka sasa jamii kuachana na imani hizo na kukubali kuwa suala la hedhi ni sehemu ya maisha ya kawaida kabisa ya msichana au mwanamke na ni jambo la baraka za Kimungu katika kuweka mfumo wa kuendeleza vizazi. Hivyo, napenda kusisitiza kuwa, tutumie maadhimisho ya mwaka huu kuhamasisha na kuwakumbusha Watanzania, Viongozi mbalimbali wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Wanahabari pamoja na jamii kwa ujumla kutambua kuwa hedhi salama ni afya na ni Baraka za uumbaji wa Mungu mwenyewe.

Nimechukua hatua ya kuvunja ukimya nawe chukua hatua hii ili kwa pamoja tuungane kuelimisha na kuhamasisha jamii kuachana na mila na desturi potofu kuhusu hedhi na kuhakikisha wanaungana kuratibu upatikanaji wa huduma na vifaa vya kujihifadhi hasa taulo za kike sehemu zote kwa makundi yote na hata kuwa na bei elekezi katika bidhaa hii.

**Ndugu Wanahabari,**

Maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama mwaka huu yanaongozwa na kauli mbiu isemayo '**Ni wakati wa kuchukua hatua ili kuhakikisha vifaa vya kujisitiri/taulo za hedhi zinapatikana kwa urahisi na bei nafuu kwa msichana/mwanamke' (It's time to take action).** Kauli mbiu hii, imekuja wakati muafaka ambapo uwezeshwaji utapelekea kuleta maendeleo na utu kwa msichana na mwanamke. Wakati huu ambao wasichana wengi kuanzia Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo pamoja na wale waliopo majumbani wanahitaji upatikanaji wa mahitaji muhimu bila kuwa na kikwazo. Ni wajibu wetu sote kuhakikisha upatikanaji wa taarifa, elimu, vifaa/taulo za kike, dawa za kupunguza maumivu kama vidonge vya **mefenamic acid** na mazingira wezeshi ya kujisitiri wakati wa hedhi. **Aidha, tutaratibu vidonge hivi vipatikane kwenye shule zote waliko mabinti zetu.**

**Ndugu Wanahabari,**

Kutokana na ongezeko la mahitaji haya ya matumizi ya Taulo za kike, natoa wito kwa watengenezaji, wauzaji na wasambazaji wa vifaa/taulo za kike, kuuza kwa bei nafuu ili kumuwezesha kila mwanamke/msichana kupata bidhaa hizi kwa urahisi huku wakizingatia ubora. Aidha, tutaratibu ajenda ya bei elekezi ya vifaa hivi bila kuathiri ubora. Hitaji hili la kuangalia bei za bidhaa hizi ni muhimu hasa tukizingatia kwamba kwenye utafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) nilioutaja hapo awali imebainika kuwa asilimia 60 ya wasichana walionekana kutomudu gharama za taulo za kike. Pia, ninawasihi watengenezaji kuweka **"package"** ya wanafunzi ili kuwapa urahisi na unafuu katika bidhaa hizi muhimu.

Pamoja na uratibu wa bei za vifaa hivi, tutaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya ndani ili kuendelea kulinda bei pamoja na kujihakikishia usalama zaidi wa vifaa hivi siku zote. Hivyo, tutakuwa na ufuatiliaji wa kuratibu wadau katika eneo hili tukienda na falsafa ya Uchumi wa Viwanda.

**Ndugu Wanahabari,**

Nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau wetu kupitia mtandao wa wadau wa Hedhi Salama (**Menstrual Health and Hygiene (MHH) Coalition**) wakiwemo Mashirika ya Kimataifa na ya Kiraia (WB, AMREF, UNICEF, UNFPA, WSSCC, Water Aid, World vision, TAWASANET, AFYA PLUS, DORICAS) na Wanachama wake, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na OR-TAMISEMI, Wanahabari, wenye viwanda vya kutengeza pedi/taulo za hedhi, wasambazaji, wahamasishaji na watumiaji. Sote tuendelee kuhamasisha upatikanaji wa vifaa vya hedhi salama ndani ya nchi na kwa sababu hiyo vipatikane kwa unafuu na ubora unaotakiwa ili kila mhitaji kwa makundi yote aweze kutumia.

**Ndugu Wanahabari,**

Wizara itaendelea kutoa elimu ya hedhi salama kwa jamii kwa lengo la kuhamasisha, kuvunja ukimya na kuachana na mila/desturi potofu kuhusu hedhi. Aidha, tutahakikisha kuwa Sera yetu ya Afya inaliweka jambo la hedhi salama kuwa moja ya vipaumbele ili kutunza heshima na utu wa mwanamke na kumpa nafasi ya kuleta maendeleo katika jamii. Napenda kutoa wito kwa Watanzania wote kuchukua hatua kuachana na mila, desturi na imani potofu juu ya masuala ya hedhi ili kuweza kuwasaidia wanawake na wasichana kuondokana na kunyanyapaliwa na kutengwa kutokana na hali ambayo Mwenyezi Mungu amewaumba nayo ili kuendeleza kizazi.

***Asanteni kwa kunisikilza.***

**Imetolewa na:**

Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb)
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,**
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**
24 Mei, 2021